**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. ENG. EVARIST NDIKILO MKUU WA MKOA WA PWANI KWENYE MAADHIMISHO YA KILELE CHA WIKI YA ELIMU NGAZI YA MKOA TAREHE 11/05/2017 KATIKA VIWANJA VYA SHULE YA MSINGI MKURANGA**

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya mliohudhuria,***
***Mhe. Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa,***
***Katibu Tawala Mkoa wa Pwani,***
***Ndugu viongozi wa Madhehebu ya Dini,***
***Makatibu Tawala Wasaidizi Mkoa,***
***Waheshimiwa, Wenyeviti Halmashauri za Mkoa wa Pwani,***
***Wakurugenzi Watendaji Halmashauri za Wilaya,***
***Wakuu wa Vitengo Mkoa,***
***Viongozi wa Idara ya Elimu Mkoa,***
***Maafisa Elimu msingi na Sekondari,***
***Mwenyekiti na Katibu wa Chama cha Walimu Mkoa wa Pwani,***
***Wakuu wa Vyuo na Taasisi mbalimbali za serikali,***
***Wakuu wa Shule Msingi na Sekondari,***
***Walimu,***
***Wanafunzi,***
***Wageni Waalikwa,***
***Waandishi wa Habari,***
***Mabibi na Mabwana.***

**ASSALAM ALLAIKUM/BWANA YESU ASIFIWE/TUMSIFU YESU KRISTO.**

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kwa ajili ya maadhimisho ya Wiki ya Elimu katika Mkoa wetu wa Pwani.

**Ndugu viongozi na wananchi,**
Siku hii ni muhimu sana kwani inatuweka pamoja sisi sote kutoka Halmashauri zote 9 za mkoa wa Pwani kujadiliana, kushirikishana na kutafakari mambo mbalimbali yanayohusu elimu katika Mkoa wetu. Ni matumaini yangu kuwa kila mmoja wetu, ataitumia vizuri fursa hii muhimu katika kujifunza mambo mbalimbali ambayo atayatumia kuboresha elimu katika eneo lake.

Aidha, nawashukuru wenyeji wetu, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwa kukubali kuwa wenyeji wa maadhimisho haya Kimkoa. Pia nawashukuru viongozi na wananchi wote wa Halmashauri za Wilaya Mkoa wa Pwani kwa mwitikio na ushiriki wenu kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha maandalizi na hatimaye maadhimisho ya siku hii. Vilevile nawashukuru viongozi mbalimbali kutoka katika Ofisi yangu kwa kuratibu vema shughuli zote zinazohusiana na maadhimisho haya.

**Ndugu viongozi na wananchi**,
Napenda pia kuipongeza serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa **Mhe. Rais Dr John Pombe Magufuli** katika juhudi za dhati za kuhakikisha kuwa elimu inaboreshwa na kuondoa baadhi ya michango isiyo ya lazima kwa utekelezaji wa Elimu bila Malipo. Ikiwa pia ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kutoa Elimu bila ya vikwazo.

**Ndugu viongozi na wananchi,**
Kaulimbiu ya Maadhimisho haya ambayo ni "**Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) ni Msingi wa Maendeleo ya Taifa**" imeandaliwa wakati muafaka na kwa hakika inaakisi dhamira na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali yetu katika kuhakikisha kuwa ubora wa elimu tunayoitoa unaanza na uimarishaji wa misingi ya stadi za KKK.

**Ndugu viongozi wote na wananchi kwa ujumla,**
Nimeona kuwa ni muhimu tukawekana sawa juu ya dhana yenyewe ya Wiki ya Elimu. Hapo awali maadhimisho kama haya yalikuwa yanalenga shughuli za Elimu ya Watu Wazima pekee na yalikuwa yakifahamika kwa jina la Juma la Elimu ya Watu Wazima. Dhana hii imeboreshwa ambapo maadhimisho haya sasa yanahusu shughuli zote za elimu; yaani kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari hadi vyuo. Pia maadhimisho haya yanahusu elimu inayotolewa katika mfumo rasmi na nje ya mfumo rasmi. Ndiyo maana shughuli tulizoziona hivi punde katika mabanda mbalimbali ya maonesho zinahusu ngazi zote hizi za elimu na kwa hakika hii ni dhamana kubwa ya maadhimisho haya kwa mfumo mzima wa elimu katika nchi yetu.

**Ndugu viongozi na wananchi,**
Katika mkoa wetu maadhimisho haya yalianza tarehe 04/05/2017 katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha na hivi leo tarehe 11/05/2017 tunahitimisha kilele chake Kimkoa katika Halmashauri hii ya Mkuranga. Ni matumaini yangu kuwa kila Halmashauri imefanya maadhimisho haya kama ilivyokuwa imeelekezwa. Maadhimisho ya Wiki ya Elimu kwa mwaka 2017 yanakusudia kutumika kutoa msukumo mpya katika kuendeleza elimu hususan uimarishaji wa umahiri wa misingi ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

**Ndugu viongozi na wananchi,**
Pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuongeza miundombinu katika shule zetu bado, tunao upungufu wa miundombinu katika shule zetu hususan vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vyoo nk. Tunahitaji Mkoa na Halmashauri kujipanga vizuri zaidi kupunguza ama kuondoa kabisa changamoto hizo katika eneo hili.

Nina imani kuwa serikali kupitia Halmashauri zake na nguvu za wananchi itaendelea kuboresha miundo katika shule mbalimbali.

Hali ya maendeleo ya elimu katika Mkoa wetu iko katika kiwango cha kuridhisha japo kuwa tunahitaji juhudi za ziada ili tuweze kufikia malengo yetu.

Pamoja na mambo mengi mazuri yanayofanyika katika sekta hii ya elimu katika Mkoa wetu, zipo chamgamoto kadha wa kadha ambazo kwa pamoja tunahitaji kujipanga na kukabiliana nazo.

Uwepo wa tafsiri potofu ya dhana ya elimu bila malipo ni miongoni mwa mambo yanayorudisha nyuma ufanisi wa kiutendaji katika sekta ya elimu kwenye mkoa wetu. Kutokana na upotofu wa tafsiri hii, wazazi na wanajamii walio wengi wanaona kuwa hawana wajibu wowote ule katika kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu katika shule zetu wakiamini kuwa hiyo ni kazi ya Serikali pekee. Tafsiri hii si sahihi na ni kikwazo katika kutekeleza dhamira ya elimu bila malipo kwenye maeneo yetu. Waraka wa elimu Na. 6 wa mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa Elimu bila Malipo umebainisha wazi wazi majukumu ya kila mdau wa elimu kama vile serikali, wazazi/walezi, walimu, Kamati/Bodi za shule na jamii kwa ujumla.

Baadhi ya majukumu yanayopaswa kutekelezwa na jamii kama yaliyobainishwa kwenye waraka huo ni kuhamasisha wazazi/walezi kuwaandikisha shule watoto wote wenye umri lengwa, kutoa ushirikiano kwa wazazi/walezi ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanahudhuria shule katika wakati wote wa masomo, kutoa ushirikiano katika shughuli zote za kuleta maendeleo ya kielimu na kuendelea kujitolea nguvu na mali ili kuleta ustawi na maendeleo ya shule zilizoko katika jamii husika.

**Ndugu Wananchi,**
Kuna baadhi ya wazazi katika jamii zetu hawana mtazamo chanya katika masuala ya elimu kwa watoto wao. Kwa mfano wapo wazazi wanadiriki kuwazuia/kuwaficha watoto wao siku za mitihani ili wasifanye mitihani hiyo ama kuwaambia watoto wao wasifanye vizuri mitihani yao. Hii inarudisha nyumba ufaulu wa shule, Wilaya na Mkoa. Nitoa rai kwenu kuhakikisha kuwa watoto wenu wanafanya mtihani na kufaulu na kuendelea na masomo yao ya juu kwani urithi mzuri kwa mtoto ni Elimu.

Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana walimu kwa kujito na kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa vizuri na wanafaulu. Lakini pia kuna baadhi ya walimu ambao hawatekelezi kikamilifu majukumu yao kwa kushindwa kuwafundisha wanafunzi ipasavyo kwa sababu mbalimbali zikiwemo za utoro, uchelewaji kazini, kutofanya maandalizi ya kutosha ya ufundishaji na ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya ualimu ni changamoto nyingine. Hii inapelekea kuwepo kwa baadhi ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi wakiwa hawajui KKK, jambo ambalo sote kwa pamoja tunahitaji kulilaani vikali. Sisi kama serikali tutaendelea kufuatilia na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa walimu wale watakaobainika kuzembea au kushindwa kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao.

Kwa upande wa sekta binafsi, inashirikiana na Serikali katika kutoa elimu kwa kuanzisha shule ambazo nyingi zinafanya vizuri na kuinua ufaulu wa Mkoa.

Ni matumaini yangu kuwa baada ya maadhimisho haya kila mmoja wetu atakuwa balozi mzuri kufikisha Kwa wengine na kuutekeleza ujumbe huu muhimu kwa maendeleo ya elimu katika shule kwa ustawi wa Taifa letu. Tanzania ya Viwanda inanza na Uimarishaji wa Sekta ya Elimu.

**Ndugu viongozi na wananchi**,

Mwisho ninawapongeza tena wale wote walioandaa maonyesho mbalimbali ambayo kwa hakika yametufunza mambo mengi na wale wote walioweza kujipatia zawadi kutokana na ushindi katika maeneo mbalimbali ya ushindani kwenye maonesho haya. Pia ninawapongeza kwa mara nyingine wale wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha maandalizi pamoja nanyi nyote mlioshiriki kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Elimu Mkoa wa Pwani.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza**